Kuwa Mwalimu wa Family Day Care:
Mambo unayohitaji kujua

SWAHILI

Novemba 2018

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.
since 1976

MKUSANYIKO WA TAARIFA ZA MWALIMU WA FAMILY DAY CARE:

Kuwa Mwalimu wa Family Day Care: Mambo unayohitaji kujua

Iwapo unafikiria kuwa, au umeombwa kuwa mwalimu wa Family Day Care, kuna mambo kadhaa unapaswa kujua ili kuhakikisha unatoa mafunzo na utunzaji wa watoto ulioidhinishwa kwa watoto wachanga nyumbani mwako.

Unapojisajili na huduma ya Family Day Care, wanapaswa kukupa mafunzo ya kina ya jinsi ya kuanza yanayojumuisha mambo kama vile kutunza watoto, kutayarisha mazoezi ya kielimu kwa watoto, afya na usalama (wako na wa watoto) na ulinzi wa watoto.

Kituo chako cha kutoa huduma kinapaswa kukusaidia kuelewa na kuzingatia Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani kuhusu ada ya msaada wa utunzaji wa watoto wanayosimamia kwa niaba ya familia zinazostahiki.

Brosha hii inatoa mukhtasari wa mambo muhimu unayohitaji kujua katika nyanja zingine kabla ya kuanza kama mwalimu kama vile - usimamizi, ada na ruzuku za serikali. Itakusaidia kuendesha huduma zako kisheria kama mwalimu. Kitakusaidia vile vile kuelewa mahitaji ya usimamizi wa msaada wa ada ya utunzaji wa watoto ambazo familia zinazostahiki zinaweza kupokea ili kuwasaidia kugharamia ada za utunzaji. Inajadili pia unachoweza na unachopaswa kutarajia kutoka kwa huduma ya Family Day Care uliyojisajili nayo.

Ulaghai na Family Day Care

Katika miaka michache iliyopita, kumekuwa na ongezeko la matukio yanayohusiana na Family Day Care ambapo walimu au huduma zimekuwa zikilaghai Serikali ya Australia ili kupata pesa huku wakitoa au wakijifanya kutoa huduma za Family Day Care. Kijitabu hiki kinanuia kuhakikisha unaepuka kujihusisha na tabia ya ulaghai au isiyozingatia sheria bila kujua.

Ada za Family Day Care

Huduma za Family Day Care hutoza ada kwa familia ili kugharamia utunzaji wa watoto. Hili hutokea kwa njia tofauti kwa kila huduma - familia zinaweza kulipa walimu moja kwa moja au zinaweza kulipa huduma, na kisha huduma kuweka pesa hizo katika akaunti ya benki ya mwalimu.

Ruzuku ya Utunzaji wa watoto

Serikali ya Australia hulipa Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto kwa familia zinazostahiki ili kuzisaidia kupunguza gharama ya ada. Vituo vya kutoa Huduma ya Family Day Care hupokea Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto kwa niaba ya familia na kisha kuipitisha kwa familia kupitia ada zilizopunguzwa.

Ruzuku ya Ziada ya Utunzaji wa Watoto

Ruzuku ya Ziada ya Utunzaji wa Watoto hulipwa kwa hali mbalimbali za familia (kwa mfano changamoto ya kifedha ya muda, kipindi cha kutoajiriwa kabla ya kupata kazi nyingine, ustawi wa mtoto, na babu na bibi ambao ni watunzaji wakuu). Kwa sababu ya hilo, ni muhimu kutoa taarifa sahihi kwa huduma ya Family Day Care kuhusu utunzaji wa watoto ambao umetoa kwa familia kwa sababu huduma itatumia taarifa hiyo kutoa ripoti kwa Serikali kuhusu utunzaji wa watoto uliotolewa kwa madhumuni ya Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto na Ruzuku ya Ziada ya Utunzaji wa Watoto.

Kanuni kuu

Msaada wa ada ya utunzaji wa watoto hulipwa kwa vituo vya kutoa huduma ya Family Day Care kwa familia zinazostahiki chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Sheria hii inazihitaji huduma za Family Day Care na walimu wao kufuata kanuni kuhakikisha kwamba msaada wa ada ya utunzaji wa watoto unalipwa kwa usahihi.

Mifano ya kanuni hizo ni:

- Watoto wote wanapaswa kurekodiwa wanapoingia na kutoka kwa utunzaji kila siku. Walimu wa Family Day Care ni lazima waweke rekodi za mahudhurio ya kila wiki ili kuonyesha watoto waliotunzwa, katika siku gani na kwa muda gani. Rekodi hizi zinahitajika ili kuthibitisha kuwa mtoto fulani ambaye alilipiwa Ruzuku wa Utunzaji wa Watoto hakika alitunzwa kwa mara zilizorekodiwa, au hakuhudhuria kwa sababu inayokubalika.
- Ripoti za vipindi zinahitaji kutumwa kwa Serikali ndani ya kipindi cha muda unaohitajika..
- Ada zote zinazolipwa kwa familia zinapaswa kutolewa risiti kwa usahihi. Familia zinahitaji kujua Ruzuku yao ya Utunzaji wa Watoto ilikuwa ya kiasi gani na walicholipa ili kuongezea kwa ruzuku waliyopata kuwawezesha kugharamia ada kamili waliyotozwa.

LAINI YA KUTOA RIPOTI

Iwapo una wasiwasi kuhusu kutokea kwatabia zisizo sahihi au zisizofaa, unaweza kuwasiliana na Idara ya Elimu na Mafunzo ya Serikali ya Australia kupitia laini yao ya kuripoti na utoe maelezo mahususi kwa 1800 664 231 au utume barua pepe kwa tipoffline@education.gov.au Unaweza kutoa ripoti bila kutaja jina lako iwapo unataka kufanya hivyo.

IWAPO JAMBO LOLOTE LINAONEKANA KUWA HALIFAI, USILIFANYE!

Je, mtu yeyote amewahi kukuambia ufanye jambo ambalo linaonekana kuwa linaweza kuwa kinyume na sheria, au lisilofaa? Labda mwalimu mwengine au mtu fulani katika huduma ya Family Day Care?   Iwapo una shaka yoyote, angalia iwapo unachoambiwa kufanya ni halali. Tuma barua pepe kwa info@fdcsupport.org.au
Unaweza pia kuwasiliana na mamlaka ya udhibiti ya jimbo lako (ikiwa ni kuhusu usalama wa mtoto au elimu) kwa **www.acecqa.gov.au/help/contact-your-regulatory-authority** au Idara ya Elimu na Mafunzo ya Serikali ya Australia kwa nambari **1800 664 231**, ikiwa ni kuhusu mitindo ya utozaji ada.

Mambo muhimu

- Family Day Care inadhibitiwa na sheria na kanuni kadhaa. Kazi zake ni:
  - kuhakikisha watoto ni salama na wanajifunza wakitunzwa na mwalimu na
  - kuhakikisha msaada wa ada ya utunzaji wa watoto unatolewa kama ada iliyopunguzwa kwa familia zinazostahiki.
- Walimu wa Family Day Care huwa wameajiriwa ama na huduma ya Family Day Care waliyojisajili nayo au huduma inawapa kandara ya utunzaji..
- Sheria na kanuni na vile vile sera na taratibu za huduma ya Family Day Care huamua jinsi utaendesha biashara yako.
- Sheria/kanuni na sera hizi huamua:
  - Jinsi huduma yako inavyoweka ada
  - Jinsi familia hutozwa ada ya huduma yako na risiti ambazo ni lazima wapate
  - Maelezo gani yanapaswa kuchukuliwa wakati wa usajili
  - Maelezo ambayo ni lazima uripoti kwa huduma ya Family Day Care kuhusu mahudhurio ya watoto na ni kwa mara ngapi unapaswa kuripoti hili
  - Bima gani unayopaswa kuchukua
  - Mifumo unayopaswa kutekeleza ili familia zitie saini wanapoleta na kuwachukua watoto kutoka kwa utunzaji wako.
- Serikali ya Asutralia hulipa Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto kwa familia zinazostahiki ili kuzisaidia kupunguza gharama ya ada za utunzaji. Walimu wa Family Day Care wana jukumu la kusaidia kuhakikisha kuwa pesa hizo zinatumiwa ipasavyo kwa:
  - kuwapa wazazi sajili ya mahudhurio ya kutia saini kila wakati wanapomleta au kumchukua mtoto wao
  - kutia saini wakati mtoto wanayemtunza hajaletwa
  - kufuata matakwa ya huduma yao kwa kuwasilisha rekodi za mahudhurio.
- Rekodi zako zinapaswa kuwa sahihi ili kuhakikisha unafuata sheria.
- Huduma za Family Day Care zinapaswa kutoa usaidizi wa aina mbalimbali kwa walimu waliojisajili nao ili kuhakikisha usimamizi unafanya kwa usahihi na kulingana na sheria. Hii ni pamoja na mafunzo ya kuanzisha, masomo ya kujiendeleza kitaaluma na usaidizi wa kila mara.
- Usijiandikishe na huduma ya Family Day Care ambayo unashuku inaweza kuwa inavunja sheria. Hii inaweza kukuweka katika hatari ya kuvunja sheria pia.
  Katu:
  - usitie saini vipindi vya mafunzo ya watoto wadogo na utunzaji wa watoto ambavyo hukutoa
  - usitie saini chochote kinachosema ulitunza watoto fulani katika siku fulani au kwa muda fulani ila kama uliwatunza
  - usiulize familia zitie sahihi chochote kinachosema ulitunza watoto wao katika muda fulani ila kama hakika ulitunza watot wao
- Iwapo utatia saini fomu au hati zingine ambazo si sahihi, unavunja sheria.

Je, msaada wa ada ya utunzaji wa watoto hufanya kazi vipi?

Msaada wa ada ya utunzaji wa watoto hutegemea iwapo familia inatimiza vigezo vyote vya kustahiki ikiwemo tathmini ya mapato ya jumla ya kila mwaka ya familia na jaribio la shughuli. Msaada wa ada ya utunzaji wa watoto kwa ujumla hulipwa moja kwa moja kwenye kituo cha kutoa huduma ili waufikishe kwa familia zinazostahiki kama ada iliyopunguzwa.

Familia hulipa kituo chao cha kutoa huduma tofauti kati ya kiasi chao cha Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto na ada inayotozwa. Ili kustahiki kwa Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto, ni lazima familia ziwe na wajibu wa kulipa ada za utunzaji wa watoto chini ya Makubaliano ya Uzingatiaji Yaliyoandikwa kati yao na mtoa huduma ya utunzaji wa watoto.

MKUSANYIKO WA TAARIFA ZA MWALIMU WA FAMILY DAY CARE:

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

This brochure has been produced in 11 languages: Amharic, Arabic, Assyrian, Dari, Dinka, French, Hazaragi, Nuer, Somali, Sudanese, and Swahili. To find the brochure in your language please go to **www.fdcsupport.org.au**

Je, ni kwa nini ninapaswa kuwaomba wazazi kutia saini kila siku wanapoleta au kukujia watoto wao?

Rekodi za mahudhurio ni hati za kishera zinazowekwa ili kuhakikisha familia zinazopokea Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto kutoka kwa Serikali ya Australia hakika zimepokea utunzaji wa watoto.

Je, kituo changu cha kutoa huduma ya utunzaji wa watoto kinapaswa kufanya nini ili kunisaidia?

Huduma yako inapaswa:

- Kukupa mafunzo ya kuanzisha kabla hujaanza kuwa mwalimu
- Kukufahamisha kwa uwazi ada na kodi wanazotoza
- Kutoa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma
- Kukutembelea mara kwa mara
- Kukusaidia kuelewa na kufuata Sheria na Kanuni za Kitaifa na kuzingatia Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani kuhusu msaada wa ada ya utunzaji wa watoto wanaosimamia kwa niaba ya familia zinazostahiki.

Kituo cha huduma nilichojisajili nacho uniuliza kila mara kutia saini mambo nisiyoyaelewa. Je, ninapaswa kukubali?

Hapana. Hakikisha kuwa unaelewa kila kitu unachokitia saini la sivyo unaweza kujipata ukivunja sheria bila kujua.

Je, Family Day Care inadhibitiwa na sheria na kanuni gani?

Kuna sheria kadhaa zinazodhibiti jinsi watoa huduma, vituo vya huduma na walimu wa Family Day Care wanavyoendesha shughuli zao. Sheria ambazo ni muhimu sana ni:

- **Sheria ya Kitaifa ya Huduma za Elimu na Utunzaji**
  www.acecqa.gov.au/national-law
- **Kanuni za Kitaifa za Huduma za Elimu na Utunzaji**
  www.acecqa.gov.au/national-regulations
- **Sheria ya Usaidizi wa Familia**
  www.education.gov.au/child-care-legislation

Kwa nini kuna sheria na kanuni nyingi?

Kutunza watoto ni kazi muhimu. Sheria na Kanuni za Kitaifa hutoa kiwango cha kitaifa cha mafunzo na utunzaji wa watoto ili kudumisha usalama wa watoto. Serikali ya Australia hutumia kiwango kikubwa cha pesa kugharamia msaada wa ada ya utunzaji wa watoto. Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani ndiyo msingi wa Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto na Ruzuku ya Ziada ya Utunzaji wa Watoto ili kupunguza ada za familia za utunzaji wa watoto.

FAHAMU MENGI ZAIDI

Mwongozo wa Utunzaji wa Watoto ni rasilimali muhimu kwa watoa huduma wa mafunzo ya awali na utunzaji wa watoto na unaweza kupatika katika:
www.education.gov.au/child-care-provider-handbook-0

Fahamu mengi zaidi kwa kutembelea tovuti zifuatazo:

- **www.education.gov.au/compliance**
- **www.fdcsupport.org.au**
- **www.education.gov.au/child-care-providers**
- **www.fdca.com.au**
- **www.acecqa.gov.au**

au kwa kuenda kwenye kituo cha huduma ya Family Day Care kilichopokaribu nawe. (Ili kupata kituo cha huduma hii kilicho karibu sana,tembelea tovuti **www.fdca.com.au** na kisha ubofye kichupo cha “find childcare”.)

Amharic በራስዎ ቋንቋ በራሪ ወረቀት ለማግኘት www.fdcsupport.org.au. ድረ ገጽን ይጎብኙ

Arabic لإيجاد الكتيب بلغتك، يُرجى تصفح موقع الويب .www.fdcsupport.org.au

Assyrian ܠܡܫܟܚܬܐ ܕܟܪܣܐ ܒܠܫܢܟ݂ ܒܥܘܬܐ ܡܢܘܟ݂ ܣܠܘܩ ܠܚܘܠܐ ܕܐܝܢܛܪܢܝܬ .www.fdcsupport.org.au

Dari برای دریافت جزوه به زبان خودتان، لطفاً به ویبسایت www.fdcsupport.org.au مراجعه کنید.

Dinka Të kɔɔr yin kitap në thoŋdu kitam tɔ̈ wëlthin ke yin lɔ në www.fdcsupport.org.au.

French Pour trouver la brochure dans votre langue, veuillez visiter le site www.fdcsupport.org.au.

Nuer Kɛ ɣöö bi ŋäc jiek rɛy warɛgakä/ kiɛ majalɛ kɛ thuok du, göa ɛ ɛn ɣöö bi wä kä www.fdcsupport.org.au.

Hazaragi برای دریافت این بروشور به زبان خود تان، لطفاً به ویب سایت www.fdcsupport.org.au مراجعه کنید.

Somali Si aad ugu heshid buugyaraha luuqadaada fadlan booqo www.fdcsupport.org.au.

Sudanese لإيجاد الكتيب بلغتك، الرجاء تصفح موقع .www.fdcsupport.org.au

Swahili Ili kupata brosha hiyo kwa lugha yako tafadhali tembelea tovuti www.fdcsupport.org.au.

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.
since 1976

Novemba 2018